
## Year 1 Phonics Screening Check

Information for parents and carers

# Ukaguzi wa Mwaka wa 1 wa Uchunguzi wa Fonetiki/Sauti

Taarifa kwa wazazi na walezi



## Fonetiki ni nini?

Fonetiki ni uhusiano kati ya herufi na sauti na ni muhimu kabisa katika kujifunza kusoma. Watoto wengine wanatatizika kujifunza kusoma, kwa hivyo ni muhimu kwamba watoto hawa watambuliwe haraka. Hivyo ndivyo, walimu wanaweza kupanga kwa msaada wowote maalum ambao wanaweza kuhitaji.

### Je! Ukaguzi wa Mwaka wa 1 wa Upimaji wa Fonetiki/Sauti ni nini?

Ukaguzi wa Mwaka wa 1 wa Uchunguzi wa Sauti ni tathmini fupi ya jimbo zima inayowaambia walimu jinsi mtoto wako anavyoendelea katika fonetiki. Ukaguzi huu wa uchunguzi unaonyesha jinsi mtoto wako anavyoweza kusoma maneno ya Kiingereza yenye michanganyiko tofauti ya herufi. Mtoto wako atakaa na mwalimu na ataulizwa kusoma maneno 40 kwa sauti. Maneno haya yanajumuisha maneno 20 halisi na maneno 20 yasiyo na maana. Kusudi la maneno yasiyo na maana ni kuona ikiwa mwanafunzi anaweza kutumia ujuzi wake wa kuchanganya ili kusoma neno badala ya kutumia kumbukumbu yake ya kuwahi kuliona neno hilo hapo awali. Kwa kawaida tathmini inachukua muda wa dakika 5 hadi 7. Ikiwa mtoto wako anatatazika mwalimu ataacha uhakiki huo. Ukaguzi huundwa kwa uangalifu ili usiwe na mafadhaiko kwa mtoto wako.

Lengo kuu la Ukaguzi wa Mwaka wa 1 wa Uchunguzi wa Sauti ni kumpa mwalimu wa mtoto wako taarifa ambayo itamwezesha kupanga kwa kujifunza kwa mtoto wako. Kila mtoto hupimwa kibinafsi na mwalimu na wanafunzi wote wa Mwaka wa 1 watatathminiwa.

### Kwa nini fonetiki ni muhimu?

Maarifa na ujuzi wa fonetiki ni muhimu sana katika kujifunza kusoma na kuandika kwa Kiingereza. Ili kufaulu, wanafunzi wanahitaji kujifunza sauti zinazoonyeshwa na herufi au michanganyiko tofauti ya herufi, na ustadi wa kuchanganya sauti hizi pamoja ili kusoma maneno. Wasomaji wanaoanza wanahitaji kujifunza jinsi ya kuchanganya sauti pamoja kwa maneno haraka na kwa ufasaha, ili wasiharibu mwendo wa usomaji na ufahamu wao wa maandishi.

Tafadhali wasiliana na shule ikiwa una maswali yoyote kuhusu Ukaguzi wa Mwaka wa 1 wa Uchunguzi wa Sauti.

### Huduma ya mkalimani wa simu

Ikiwa unahitaji usaidizi wa mkalimani ili kuwasiliana na shule, tafadhali pigia simu kwa 131 450, mwambia opereta ni lugha gani unayohitaji na mwuliza apige simu shuleni. Opereta atapata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia kwa mazungumzo yako. Hutatozwa kwa huduma hii.



NSW GOVERNMENT